

# Je, unajua sehemu rasmi za kuripoti matukio ya ukatili wa kijinsia?

## SIKU 16 ZA UANAHARAKATI DHIDI YA UKATILI WA KIJINSIA

### KAULI MBIU: CHAGUA KUTOKOMEZA UKATILI WA KIJINSIA

#### UTANGULIZI

Mtandao wa Kupambana na Ukatili wa Kijinsia (MKUKI) kwa kushirikiana na Asasi za Kiraia (AZAKI) umekuwa mstari wa mbele kuhamasisha jamii kutokomeza ukatili wa kijinsia ili kufanikisha usawa, amani, na maendeleo jumuishi. Hata hivyo, vitendo vya ukatili bado vinaendelea, huku matukio mengi yakiripotiwa kwa kiwango kidogo kwenye vyombo vya sheria. Wakati mwingine, migogoro hutatuliwa nyumbani, jambo linalowanyima wahanga haki yao ya msingi na kuchochea madhara zaidi.

Kijarida hiki kinatoa mwongozo kuhusu sehemu rasmi za kutoa taarifa za ukatili wa kijinsia. Kila tukio linapaswa kuripotiwa kwenye mamlaka zinazohusika ili kusaidia wahanga na kuhakikisha wahalifu wanawajibishwa.

**Ukatili wa kijinsia unazuilika!** Ungana nasi katika kuimarisha jamii isiyo na ukatili kwa kuripoti matukio na kusaidia wahanga kufikia haki.

#### Dawati la Jinsia na Watoto - Jeshi la Polisi

Dawati hili limeanzishwa mahsusi kushughulikia masuala ya ukatili wa kijinsia. Ukifanyiwa au kushuhudia ukatili, unaweza kutoa taarifa kwa hatua zifuatazo:

## Hatua za Kufuatilia:

1. Tembelea kituo cha polisi na omba kuonana na afisa wa Dawati la Jinsia.
2. Toa maelezo sahihi ya tukio, na hakikisha yanachukuliwa rasmi kwenye jalada la uchunguzi.
3. Mkabidhi afisa vielelezo vyote vya tukio (kama nguo au vitu vingine vilivyohusika).
4. Omba Fomu ya Polisi Namba Tatu (PF.3) kwa matibabu iwapo ulipata madhara. Fomu hii ni muhimu pia wakati wa ushahidi.
5. Hakikisha maelezo yako yanahakikiwa kabla ya kutia saini.

## Iwapo ni Ukatili wa Kingono (Ubakaji/ Ulawiti):

- Usifue au kubadilisha nguo mara baada ya tukio.
- Hifadhi nguo kwenye mfuko wa karatasi; epuka mifuko ya plastiki.
- Usichane nywele wala kuoga kabla ya uchunguzi.

## Vituo vya Afya

Kwa hali ya dharura, unaweza kwenda moja kwa moja kwenye kituo cha afya:

## Hatua za Kufuatilia:

1. Wahi kituoni ndani ya masaa 72 kwa matibabu ya haraka.
2. Fanya vipimo vya kiafya ili kubaini athari na kupatiwa matibabu stahiki.
3. Ombadawaza kuzuia maambukizi ya VVU na mimba zisizotarajiwa iwapo ni tukio la ubakaji.

4. Peleka PF.3 kwa daktari kwa huduma za kitabibu.

## Shule

Walimu walezi wamepewa jukumu la kusaidia kushughulikia matukio ya ukatili dhidi ya wanafunzi.

## Hatua za Kufuatilia:

1. Toa taarifa kwa mwalimu mlezi au mwalimu mkuu.
2. Omba msaada wa kufika Dawati la Jinsia, kituo cha afya, au ofisi ya ustawi wa jamii.
3. Ikiwa unahofia kuripoti, unaweza kuomba msaada kutoka kwa mwanafunzi mwenzako unayemuamini.

## Ofisi ya Ustawi wa Jamii

Idara ya Ustawi wa Jamii inahusika moja kwa moja na masuala ya watoto na watu walio kwenye mazingira magumu.

## Hatua za Kufuatilia:

1. Wasiliana na maafisa ustawi wa jamii kwa msaada wa kuripoti polisi na kupata huduma nyinginezo.
2. Omba msaada wa hifadhi salama kwa mtoto au mhanga endapo usalama uko mashakani.

## Serikali za Mitaa

Viongozi wa serikali za mitaa ni kiungo muhimu katika kushughulikia ukatili wa kijinsia.

## Hatua za Kufuatilia:

1. Toa taarifa kwa kiongozi wa mtaa au kijiji.
2. Omba msaada wa kufika polisi au kituo cha afya.

3. Wajulishe ikiwa tukio linaendelea kwa hatua za uokozi.

### Vituo vya Msaada wa Kisheria

Vituo vya msaada wa kisheria hutoa huduma bure kwa wahanga wa ukatili wa kijinsia na kuwasaidia kupata haki.

#### Hatua za Kufuatilia:

1. Wasiliana na afisa wa msaada wa sheria kwa maelezo.
2. Omba msaada wa kuunganishwa na polisi, huduma za afya, au hifadhi salama.

#### Huduma za Dharura

Piga simu kwa namba zifuatazo:

- **112:** Polisi kwa dharura.
- **113:** TAKUKURU (matukio ya rushwa ya ngono).
- **114:** Matukio ya majanga (moto, mafuriko, n.k.).
- **115:** Gari la wagonjwa.
- **116:** Ukatili dhidi ya watoto.

#### Mifumo ya Mtandaoni:

Pakua programu zifuatazo kwa msaada wa kisheria:

- *Funguka App*
- *Haki Kiganjani*
- *Sheria Kiganjani*
- *Haki Yangu*

### Wasiliana Nasi

Kwa msaada zaidi, wasiliana na mashirika yafuatayo bila malipo:

- **WiLDAF:** 0800780070
- **LHRC:** 0800750035
- **TAWLA:** 0700751010
- **WLAC:** 0800780100
- **C-Sema:** 116

### Tuchukue Hatua!

Pamoja tunaweza kuzuia ukatili wa kijinsia. Ripoti matukio na linda haki za wahanga!

# SIKU



## ZA UANAHARAKATI DHIDI YA UKATILI WA KIJINSIA



**WILDAF**  
TANZANIA

Women in Law & Development Africa



### MAWASILIANO:-

Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Barani Afrika (WILDAF)  
Mikocheni "A", Mtaa wa WILDAF,  
Jengo F, Kitalu Na. 635, S.L.P 76215, Dar es Salaam - Tanzania

**Simu Na:** 255 022 2701995

**Barua pepe:** [info@wildaftanzania.or.tz](mailto:info@wildaftanzania.or.tz)

**Tovuti:** [www.wildaftanzania.or.tz](http://www.wildaftanzania.or.tz) | **Mitandao ya kijamii:** @willdaftz